رساله حقوق

امام سجاد علیه السلام

RISALATUL HUQUQ

RISALA YA HAKI ZA BINADAMU

Risalatul Huquq

Kwa Ushirikiano : Wa Abolfazl Hajializadeh

Ahlal-Bayt During Bunge

www.ahl-ul-bayt.org

info@ahl-ul-bayt.org

FAHARASA:

UTANGULIZI: 5

DIBAJI: 9

RISALA YA HAKI ZA BINADAMU. 11

1. HAKI YA MWENYEZI MUNGU: 11

2. HAKI YA NAFSI: 11

HAKI YA VIUNGO: 12

3. HAKI YA ULIMI: 12

4. HAKI YA MASIKIO: 12

5. HAKI YA MACHO: 12

6. HAKI YA MIGUU: 13

7. HAKI YA MIKONO: 13

8. HAKI YA TUMBO: 13

9. HAKI YA TUPU ZAKO: 14

HAKI ZA MATENDO: 14

10. HAKI YA SALA: 14

11. HAKI YA FUNGA: 14

12. HAKI YA SADAKA: 15

13. HAKI YA KAFARA: 16

HAKI ZA VIONGOZI: 17

14. HAKI YA MTAWALA: 17

15. HAKI YA MWALIMU: 17

16. HAKI YA TAJIRI WAKO: 18

WATU WALIO CHINI YA MAMLAKA YAKO: 18

17. HAKI ZA RAIA: 18

18. HAKI YA MWANAFUNZI: 19

19. HAKI YA MKE: 19

20. HAKI YA MTUMISHI: 20

HAKI YA NDUGU NA JAMAA: 21

21. HAKI YA MAMA: 21

22. HAKI YA BABA: 22

23. HAKI YA MTOTO: 22

24. HAKI YA NDUGU: 23

25. HAKI YA ALIYEKUFANYIA HISANI: 23
26. HAKI YA ALIYEFANYIWA HISANI: 23
27. HAKI YA MFADHILI: 24
28. HAKI YA MUADHINI: 24
29. HAKI YA IMAMU: 25
30. HAKI YA MWENZI: 25
31. HAKI YA JIRANI: 26
32. HAKI YA SWAHIBA: 26
33. HAKI YA MSHIRIKA: 27
34. HAKI YA UTAJIRI: 27
35. HAKI YA MWENYE KUDAI: 28
36. HAKI YA UNAEISHI NAYE: 28
37. HAKI YA MSHTAKI: 28
38. HAKI YA MSHITAKIWA: 29
39. HAKI YA MWENYE KUOMBA USHAURI: 30
40. HAKI YA MSHAURI: 30
41. HAKI YA MWENYE KUOMBA NASAHA: 31
42. HAKI YA MWENYE KUTOA NASAHA: 31
43. HAKI YA WAKUBWA ZAKO: 32
44. HAKI YA WADOGO ZAKO: 32
45. HAKI YA MWENYE KUOMBA MSAADA: 33
46. HAKI YA UNAYE MUOMBA MSAADA: 33
47. HAKI YA MWENYE KUKUFURAHISHA: 34
48. HAKI YA ALIYEKUTENDEA UBAYA: 34
49. HAKI ZA WAISLAMU: 35
50. HAKI YA WASIO KUWA WAISLAMU: 36

بسم الله الرحمن الرحيم

Naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma mwenye kurehemu.

UTANGULIZI:

Moja kati ya matatizo yanayosumbua na kushughulisha akili ya mwanadamu tangu, awali mpaka hivi sasa, ni suala la utetezi na ulinzi wa haki za binadamu. Umuhimu wa suala hili, umepelekea kuandikwe, makala na vitabu kadha wa kadhaa vikizungumzia haki za binadamu, vikielezea kanuni na kubainisha kauli na nadharia za kuwahamasisha watu kulinda na kuchunga haki za binadamu. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, suala la haki za binadamu, limeshikiliwa na nguvu za utawala ambazo zinatumia, tasisi za haki za binadamu kama silaha ya kuwakandamiza na kuwapokonya haki wanyonge na wasiojiweza. Na hapa ndio tunaona kwamba, taasisi nyingi zinazosimamia haki za binadamu, zinadai kuwa zinatetea haki za binadamu, lakini hawana utetezi wowote, bali hii ni njia tu ya kujipatia manufaa kwa urahisi. Na hivi ndivyo tunavyoona katika maisha yetu ya kila siku, mataifa yenye nguvu ya kimagharibi na Marekani na washirika wao wakitumia vibaya taasisi za kuchunga haki za binadamu.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, taasisi za haki za binadamu, zinazodai na kunadi kutetea haki za binadamu, mpaka sasa zimeshindwa kutetea haki za binadamu kama inavyotakiwa, bali zimeshindwa kutetea hata haki za watu wanaonewa na kudhulumiwa, hii inatokana na kwamba, wao wenyewe ndio wanaokiuka haki za binadamu, hivyo inakuwa ni vigumu kwao kutetea na kutekeleza haki za wengine.

Dini ya kiislamu ni moja kati ya dini zilizojuu katika kilele cha tabia na maadili, dini hii inasheria na mafunzo mengi yanayohusiana na kuhimiza kulinda maadili binafsi na maadili ya jamii kwa ujumla. Na kuna maandiko ya aya na riwaya

nyingi zinazo ongelea haki za wanadamu, kutafuta haki, kukubali haki, kusisitiza watu kusema haki, kuwa wasafi wa nia katika kuitafuta haki na kuhamasisha kushikamana na haki na misingi yake.

Amirul mu'uminin Ali bin Abi Twalib anasema:
Kushirikiana katika kusimamisha haki, ni amana.[1]
Kitabu hiki cha risala za haki za Binadamu ambayo kiko mikononi mwako hivi sasa, ni moja kati ya mafunzo na mirathi za pekee za dhehebu la Shia.
Risala hii ina kusanya na kuzungumzia aina hamsini za haki za binadamu, na wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu mtukufu na wajibu wao wa kimaadili. Haki hizi zimegawanywa katika milango saba:
Mlango wa kwanza: haki za Mwenyezi Mungu.
Mlango wa pili: haki ya nafsi na viungo vya mwili.
Mlango wa tatu: haki za matendo na ibada.
Mlango wa nne: haki za raia na watawala.
Mlango wa tano: haki za ndugu.
Mlango wa sita: badhi ya haki za kijamii.
Mlango wa saba: haki za mali.
Haki za Mwenyezi Mungu na maswala yanayohusu maadili yaliyozungumziwa katika kitabu hiki, kinacho bainisha haki kwa kulinda maadili ya kibinadamu ni pamoja na: Haki ya Mwenyezi Mungu, haki ya nafsi, haki ya ulimi, haki ya masikio,haki ya macho, haki ya mikono, haki ya miguu, haki ya tumbo,haki ya tupu, haki ya sala, haki ya hijja,haki ya swaumu,haki ya sadaka, haki ya kiongozi, haki ya imamu na watawala haki ya mwalimu na mwanafunzi, haki ya wazazi, haki ya mtoto, haki za raia kwa mtawala, haki ya mke, haki ya wafanyakazi, haki ya

[1] Uyunul hikam wal mawaidh hadithi ya 5563

ndugu,haki ya mwenye kusaidia, haki ya muadhini, haki ya imamu wa sala, haki ya jirani, haki ya rafiki, haki ya mshirika, haki ya mali,haki ya mwenye kudai, haki ya mwenye kushtaki na mwenye kushtakiwa,haki ya mwenye kuomba ushauri, haki ya mwenye kutoa ushauri, haki ya mwenye kutoa nasaha, haki ya mwenye kupewa nasaha, haki za wakubwa, haki za wadogo, haki za mwenye kuomba msaada, haki ya mwenye kukupa siri, haki za waislamu na haki ya wasiokuwa waislamu.

Tunataraji kwamba risala hii, yenye thamani ambayo kwa muda mrefu imekuwa ni rejea na kigezo cha pekee katika maisha ya kila siku ya mashia, wanazuoni wa shia, wafuasi wa shia, wapenzi wa haki na wapenzi wa kizazi cha mtume Muhammad s.a.w. itakuwa ni msaada mkubwa kwako.

Tunataraji risala hii, isajiliwe katika taasisi za umoja wa mataifa kama hati maalum ya kutetea haki za binadamu, na iwe ndio njia ya wanaotafuta elimu na kutaka kujua haki za binadamu kwa mujibu wa mafunzo matukufu ya mtume Muhammad s.a.w na kizazi chake kitukufu.

Na katika kuhitimisha napenda kutuma salamu zangu kwa imam mtukufu, ambaye aliendesha mapinduzi na kufungua akili na kuwaamsha wanadamu walio lala naye si mwingine bali ni Imam Husein bin Ali bin Abi Twalib a.s, kwani amevumilia na kustahamili matatizo, taabu na mashaka mengi ili ujumbe na wito wa haki uwafikie walimwengu wote na kuwaamsha waliolala na kutikisa ngome za madhalimu na kuendeza haki katika ulimwengu.

Salamu na amani ziwafikie wapenda haki na watafuta haki na wanafunzi wa kweli wa imam Sajjad Ali bin Husein (Zainul abidin) ambaye alitumia muda wake mwingi kufanya ibada hata akajikuta anapata alama za kusujudu katika kila sehem ya mwili wake inayogusa chini wakati wa kusujudu, ambaye amezungumziwa na

na Imam Swadiq a.s akisema: siku ya Qiyama atanadi mwenye kunadi na kusema: Yu wapi Zainul abidin, naye ataitika na kuzipangua safu akielekea alikoitwa.[2]

Muhammad Salar[3]

[2] Mizanul hikma hadithi ya 1131

[3] Hujatul islam walmuslimin Muhammad Salar ni mwanafikra na mchambuzi wa elimu ya dini, ni katika watu wenye harakati katika masuala ya kidini na kitamaduni, ambaye kwa sasa ni mkuu wa Taasisi ya kimataifa ya Ahlul bayt a,s.

DIBAJI:

Wajibu na haki ya awali na ya asili ni haki ya Mwenyenzi Mungu kwako, kwani yeye ndiye aliyekuumba na kuweweka hapo ulipo,haki ya Mwenyezi Mungu ndio haki kuu na haki nyingine ni matawi ya haki hiyo, haki nyingine ni haki yako wewe ambayo inakuhusu wewe na mazingira yako yote kwa ujumla.

Mwenyezi Mungu mtukufu, amevipa viungo vyako haki na misingi maalum ya kuifuata; macho yana haki yake,masikio yana haki yake,ulimi una haki yake,mikono ina haki yake,miguu ina haki yake,tumbo lina haki yake na tupu zina haki yake, viungo hivi saba ndiyo viungo ambavyo kwa kawaida mwanadamu huvitumia katika matendo na amali zake za kila siku.

Kisha Mwenyezi Mungu amezipitia amali zako haki kwako, sala ina haki yake kwako, saumu ina haki yake kwako, sadaka ina haki yake kwako, hadiya ina haki yake kwako na matendo yako mengine yote, Mwenyezi Mungu mtukufu, ameyawekea haki zake kwako.

Kisha tunahama kutoka kwenye haki zako kuelekea kwenye haki za wenzako, ambapo katika hao kuna wenye haki za wajibu kwako, mfano wa haki za Mitume na Maimamu kwako na haki za ndugu jamaa na rafiki zako.

Haki hizi tulizo zitaja ndio asasi na msingi waa haki za binadamu, na haki nyingine zote zinatokana au ni sehemu ya haki hizi:

Haki za viongozi; ziko katika mafungu matatu: haki za viongozi wako, haki ya walimu wako na haki za walezi wako.

Haki za raia; ziko katika mafungu matatu: haki ya raia kwa kiongozi, haki ya mwanafunzi kwa mwalimu, na haki ya watu kwa walezi wao.

Watu walio chini ya mamlaka yako kama vile watumishi, mke na watoto wote wanahaki zao kwako,

Ndugu zako na watu wako wa karibu pia wanahaki zao kwako, ambapo mwenye haki zaidi kwako ni mama yako, kisha baba yako, kisha kaka na dada zako na kisha haki za ndugu wengine, ambapo aliyekaribu zaidi ana haki zaidi.

Kisha kuna haki ya wakuu wako wa kazi, haki ya wafanya kazi wako, haki ya waliokufanyia hisani, haki ya muadhini, haki ya imamu na haki ya maamuma wenzako.

Kisha kuna haki ya jirani, haki ya swahiba, haki ya mshirika, haki ya tajiri, haki ya mtu unayemdai, haki ya anayekudai, haki ya unaoishi nao, haki ya mshauri na haki ya mwenye kukuomba ushauri.

Kisha haki ya mwenye kukuomba nasaha na haki ya mtoa nasaha na kunasihi, haki ya wakubwa zako na haki ya wadogo zako, haki ya mwenye kukuomba na haki ya unayemuomba, haki ya aliyekutendea wema na aliyekutendea ubaya, ima kwa makusudi au bahati mbaya, haki ya waislamu wenzako na haki ya wasio kuwa waislamu kwako, haki kwa majanga na mabalaa yanayowasibu watu.

Basi ni faida iliyoje kwa yule mwenye kutekeleza haki za binadamu na kutekeleza wajibu wake aliyowekewa na Mwenyezu Mungu mtukufu.

Kitabu hiki kinaelezea haki za binadamu kutoka katika mafunzo ya imam Sajjad ambaye ni maarufu kama Imam Zainul Abidin ambaye ni mjukuu wa mtume Muhammad s.a.w[4] ambaye pia ni imamu wa nne wa dhehebu la kiislamu la Shia ithna asharia.

Katika kitabu hiki Imam Zainul Abidin ametufundisha haki za binadamu hamsini.

Natumai kitabu hiki kitakuwa ni muongozo sahihi kwa wapenda haki kote ulimwenguni.

[4] S.a.w = Swalla llahu alai wa alihi.

RISALA YA HAKI ZA BINADAMU.

Sheikhul faqiih, Abu Jaafar Muhammad bin Ali Hussein bin Musa bin Babawayh Qummi almaarufu kama Sheikh Swaduq ametuhadithia kwamba: Ali bin Ahmad bin Musa ametuhadithia kwamba: Muhammad bin Jaafar Kufiyul asadi ametuhabarisha kwamba: Muhammad bin Ismail Barmaki ametuambia, akisema kwamba: Ismail bin Fadhil amepokea toka kwa Thabit bin Dinar thamali, kutoka kwa Imam Ali binil Husein bin Ali bin Abitwalib Zainul abidin a.s kwamba amesema:

1. HAKI YA MWENYEZI MUNGU:

   Haki ya asili na iliyokuu kwako, ni haki ya Mwenyezi Mungu, kwamba: unapaswa umwabudu bila ya kumshirikisha, ikiwa utamwabudu kwa unyenyekuve, nia safi na ikhlasi basi Mwenyezi Mungu mtukufu , atakupa uwezo wa kujitosheleza na kutohitajia mtu hapa duniani na akhera na atakupa na kukuhifadhia kila ukipendacho.

2. HAKI YA NAFSI:

   Haki ya nafsi yako, nikwamba: yakupasa uitumie nafsi yako na nguvu zako zote kumtii Mwenyezi Mungu mtukufu. Na utekeleze haki ya ulimi wako, masikio yako, macho yako, mikono yako, miguu yako, tumbo lako, na tupu zako, na wakati wa kutekeleza haki hizi utafute msaada kwa Mwenyezi Mungu ili ufanikishe wajibu wako vyema.

HAKI YA VIUNGO:

3. HAKI YA ULIMI:

   Haki ya ulimi wako, ni kwamba: usiutumie kuzungumza yasiyo na faida, na uuzoeshe kuzungumza mambo mema yenye faida, uuzoeshe wema na kauli njema kwa watu. Na uwe kimya isipokuwa uzungumze sehemu ambapo kuna haja na ulazima wa kuzungumza, na kwenye manufaa katika maisha yako ya dunia na akhera, na uuepushe ulimi wako na kuzungumza upuuzi na mambo yasiyokuwa na faida ambayo yanaweza kukusababishia madhara na hasara kubwa.

   Akili na maandiko pia vimetoa ushahidi juu ya madhara ya ulimi ikiwa utatumika vibaya, kwani kwa kupitia ulimi unafahamika uwezo wa akili ya mtu. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

4. HAKI YA MASIKIO:

   Haki ya masikio, ni kwamba: uyaepushe na kusikia masengenyo,na uuepushe na kusikia kila kisichofaa kusikia, na badala yake uwe msikivu wa mema yenye kupendeza, Kwani masikio ndio njia inayopeleka athari za mazungumzo katika moyo na akili yako, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

5. HAKI YA MACHO:

   Haki ya macho ni kwamba: usiyatumie kutazama mambo yasiyo halali kwako, na badala yake uyatumie kutazama mambo mema yenye mafunzo na faida kwako.

6. HAKI YA MIGUU:

   Haki ya miguu yako ni kwamba: usitumie kwenda katika yale yasiyohalali kwako, na usiitumie kama usafiri wa kukupeleka kwenye mambo ya fedheha na aibu kwako, basi itumie kama usafiri wa kukufikisha kwenye manufaa ya duniani na akhera, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

7. HAKI YA MIKONO:

   Haki ya mikono yako ni kwamba: usiitumie isipokuwa katika mambo ya halali, laa sivyo utapata adhabu kali ya Mwenyezi Mungu huko Akhera, na pia utaambulia lawama za watu katika ulimwengu huu, Na katu usiizuie mikono yako kufanya matendo ambayo Mwenyezi Mungu mtukufu amekuamrisha kuyafanya.

   Na unapaswa uitumie mikono yako katika mambo yenye utukufu, Kwa kuitimia kufanya kila chenye faida na manufaa, ukifanya hivyo utaheshimika duniani na utapata thawabu na ujira mzuri akhera.

8. HAKI YA TUMBO:

   Haki ya tumbo lako ni kwamba: ulifanye tumbo lako kuwa ni chombo au sehemu ya kukusanyika vitu vya haramu sawa sawa iwe vichache au vingi,bali hata katika vyakula vya halali pia uwe na kipimo, kula kwa kiwango kinacho hitajika, na usile kwa kujaza tumbo na kufanya israfu, usisahau kipimo na kula kwa wastani na uchunge adabu, heshima na taadhima wakati wa kula. Imethibika kuwa, kula sana ndio sababu ya mtu kuwa mzembe na mvivu, ambapo hupelekea kukufanya kuwa mzito, katika kufanya amali na matendo mema, pia kula sana kuna sababisha ujinga na akili kusinzia na kulemaa.

9. HAKI YA TUPU ZAKO:

Haki za tupu zako ni kwamba: unatakiwa uzihifadhi na kuuzuia kutenda mambo ya haramu, na ili uzihifadhi na mambo ya haramu unatakiwa kuyahifadhi macho yako kutokana na kutazama mambo ya haramu, kwani macho yanahisa kubwa sana katika kumfanya mtu atumbukie kwenye maovu, pia jitahidi kukumbuka mauti, Muongope Mwenyezi Mungu mtukufu, ogopa ghadhabu na adhabu za Mwenyezi Mungu mtukufu, usitegemee watu na umtegemee Mwenyezi Mungu mtukufu pekee, kwani hakuna nguvu wala utukufu isipokuwa ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

HAKI ZA MATENDO:

10.HAKI YA SALA:

Haki ya sala ni kwamba: unatakiwa ufahamu kuwa, uko mbele ya uangalizi wa Mwenyenzi Mungu mtukufu na kwamba wakati wa sala unasimama mbele za Mwenyezi Mungu, mjuzi mwenye kuona na kutambua dhahiri na yaliyofichika,utakapolitambua jambo hili, unatakiwa kuwa mja mnyenyekevu na mwenye hamu ya kupokea rehema za Mwenyezi Mungu mtukufu, ukihofu na kuogopa ghadhabu na adhabu za Mwenyezi Mungu mtukufu,ukiwa mwenye matarajio ya kupata unachokiomba, kutokana na huruma na ukarimu wa Mwenyezi Mungu mtukufu, ukiwa makini, mnyenyekevu na mtulivu, ukiomba msamaha na kuachwa huru kutokana na kifungo cha madhambi uliyokuwa nayo, madhambi ambayo yamekupeleka kwenye maangamio,kwani hakuna nguvu wala kimbilio ila kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

11.HAKI YA FUNGA:

Haki ya funga ni kwamba unatakiwa ufahamu kuwa: Funga ni pazia na kizuizi cha moto wa Jahannam, ambacho Mwenyezi Mungu mtukufu amekuwekea kwenye ulimi wako, masikio yako, macho yako,tupu zako, na tumbo lako.

Mtume Muhammad s.a.w anasemema: “Funga ni ngao inayokukinga na moto mkali wa Jahannam”,

hivyo kama utadumu kuwa ndani ya kizuizi na pazia hilo, alilokuwekea Mwenyezi Mungu mtukufu, basi hapana shaka utakuwa umejikinga na moto mkali wa Jahannam, na ikiwa hauta itumia vizuri ngao na pazia hii aliyokupatia Mwenyenzi Mungu mtukufu, basi fahamu kuwa hautakuwa katika amani wala kinga ya moto wa Jahannam, Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

12.HAKI YA SADAKA:

Haki ya sadaka ni kwamba: unatakiwa ufahamu kuwa, sadaka ni hazina na akiba yako unayoiweka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, hazina ambayo haihitaji shahidi kinyume na Mwenyezi Mungu mtukufu, utakapofahamu jambo hilo unatakiwa kuwa na matumaini zaidi kwa ile hazina uliyo ihifadhi kwa siri na mbali ya macho ya watu, kuliko ile uliyoihifadhi hadharani, hivyo fahamu kutoa sadaka Mwenyezi Mungu pekee, akakushuhudia ni bora zaidi kuliko kutoa hadharani watu wakakushuhudia.

Hivyo unapokuwa unataka kutoa kitu kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu mtukufu, ni vyema ukatoa kwa siri, na ujiepushe na kutoa hadharani ili watu wakuone au kujitangaza kuwa nawe umetoa sadaka, iwe ni siri yako wewe na Mola wako, usitangaze wala kutoa hadharani, kwani Mwenyezi Mungu mtukufu, haitaji shahidi kukulipa amana yako.

Na wakati wowote utakapo bahatika kutoa sadaka, jiepushe na masimango au matangazo ya kukufanya uonekane umetenda wema, kwani kufanya hivyo si kujitukuza, bali kujishusha, masimango na matangazo, wakati wakutoa sadaka au baada ya kutoa sadaka ni ishara tosha ya kuwa hujatoa sadaka kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu mtukufu, bali utakuwa umetoa kwa ajili ya umaarufu au vitu vingine. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

13.HAKI YA KAFARA:

Haki ya kafara ni kwamba: mnyama na kafara unayoitoa itolewe kwa nia safi, ukitaraji malipo na rehema za Mwenyezi Mungu mtukufu, na si kufanya hivyo kwa kutaraji kupata sifa toka kwa watu, basi kama utatoa kafara yako kwa kuzingatia masharti haya, hapana shaka utakuwa umetoa kwa ajili ya kujiweka karibu na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu mtukufu kwa huruma zake, atakulipa na kuwa radhi nawe.

Hivyo fahamu kwamba Mwenyezi Mungu, ameweka njia nyepesi kwa waja wake wanaomuhitajia wala hakuweka njia ngumu kwa wajawake, na ndio maana amewawekea waja wake kanuni na sheria nyepesi kuzitekeleza wala hajawawekea kanuni na sheria ngumu, hivyo wakati wa kutoa kafara toa kwa unyenyekevu na upole kwa ajili ya kutaka radhi za Mwenyezi Mungu mtukufu.

HAKI ZA VIONGOZI:

14. HAKI YA MTAWALA:

Haki ya mtawala ni kwamba; unapaswa utambue kuwa wewe ni sehemu ya jaribio kwake, na kwamba mtawala anajaribiwa na kutahiniwa na Mwenyezi Mungu mtukufu kutokana na madaraka na mamlaka aliyonayo kwako. Basi kuwa mtiifu kwake na usiwe muasi isije ikawa ni sababu ya wewe na yeye kupata madhara, kuwa mtiifu kwake lakini utiifu usizidi kiasi cha kumuasi Mwenyezi Mungu mtukufu na kuvuka mipaka ya sheria ya Mwenyezi Mungu mtukufu, na usimchukie yeye na utawala wake bila sababu za msingi, kwani ukifanya hivyo utakuwa umejisababishia matatizo wewe mwenyewe,pia unatakiwa usaidiane na utawala wake katika kutekeleza majukumu. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

15. HAKI YA MWALIMU:

Haki ya mwalimu ni kwamba unatakiwa kumheshimu, ukae kwa heshima uwapo mbele yake na umsikilize kwa utulivu na umakini, na kutumia akili na fikra na moyo safi katika kumsikiliza na ujiepushe na kuhama kifikra au kufikiria mambo ya anasa ili akupatie elimu.

Pia yakupasa kutambua kuwa wewe ni kama mjumbe wa mwalimu wako, na unatakiwa uliyofundishwa uyafikishe na kuwafundisha wasiojua, na unatakiwa ufikishe ujumbe na kuifundisha elimu hiyo kama ulivyoipokea toka kwa mwalimu wako, bila ya kuongeza yasokuwepo au kupunguza yalokuwepo, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

16.HAKI YA TAJIRI WAKO:

Haki ya tajiri wako ni kwamba: unatakiwa ufahamu kuwa tajiri wako anahaki kama ya mtawala wako, tofauti ni kwamba tajiri yuko ana haki na mamlaka ya karibu zaidi kwako kuliko watawala wako, ambao utawala wao ni kwa raia wote,hivyo unapaswa kumtii katika masuala makuu na ya kawaida ambayo hayakinzani na amri ya Mwenyezi Mungu mtukufu, wala hayakuzuii kutimiza wajibu wako ambao Mwenyezi Mungu mtukufu ameuweka kwa waja wake, hivyo, unawajibu wa kumtii tajiri wako katika mambo ambayo hayakinzani na amri wa Mwenyezi Mungu mtukufu na wala haya kiuki haki za binadamu na viumbe wengine.

WATU WALIO CHINI YA MAMLAKA YAKO:

17.HAKI ZA RAIA:

Haki za raia ni kwamba: unatakiwa ufahamu kwamba, wewe ni mtawala na una mamlaka na madaraka kwa raia wako, na kwamba raia wako wanahaki kutoka kwako, na unatakiwa ufahamu kwamba nguvu na utawala ulionao unatokana na raia hao dhaifu. Hivyo unatakiwa ulinde na kuchunga maslahi ya watu hawa dhaifu, ambao wamekupa utawala na madaraka ya kuhukumu, basi wapatie haki zao na wala usiwaonee wala kuwakandamiza kwa kuwa ni madhaifu wasio na nguvu.

Na unatakawa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, kwa kukupatia neema na madaraka ulonayo, kwani Mwenyezi Mungu huwalipa mema na kuwazidishia neema waja wake wenye kutambua na kushuru kwa neema

walizopewa na Mwenyezi Mungu mtukufu. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

18.HAKI YA MWANAFUNZI:

Haki ya mwanafunzi ni kwamba: ukiwa kama mwalimu unatakiwa ufahamu kwamba, Mwenyezi Mungu mtukufu amekutukuza na kukupa cheo kwa wanafunzi wako, kutokana na elimu na hazina ya hekima aliyokupatia, hivyo ikiwa utakuwa mpole, mwenye huruma na hisani kwa wanafunzi wako,na ukawalea na kuwafundisha wanafunzi wako kwa huruma na kuwapa nasaha na mafunzo mema na ukawa na subira na uvumilivu katika kuwafundisha, kuwaelimisha na kuwaelewesha na ukatumia vizuri hazina ya hekima na elimu aliyokupatia Mwenyezi Mungu mtukufu, katika kuwafundisha na kuwatoa wanafunzi wako katika janga la kiza, ujahili na ujinga, basi wewe utakuwa ni mwalimu aliyeongoka na mwenye kuongoza na utakuwa ni mtumishi bora wa jamii.

Ama ikiwa utakwenda kinyume na maadili na ukanyima na kuwa bahili wa elimu kwa wengine basi utakuwa umefanya hiana na umetumia vibaya hazina ya elimu na uwezo aliokupatia Mwenyezi Mungu mtukufu.

19.HAKI YA MKE:

Haki ya mke ni kwamba: mume anatakiwa afahamu kwamba, mkewe ni mshirika, rafiki na msaidizi ambaye Mwenyezi Mungu mtukufu amempatia ili apate utulivu na usawa katika maisha yake, hivyo inawapasa mume na mke wafahamu umuhimu wa neema ambayo Mwenyezi Mungu mtukufu amewapatia, na waishi na kushirikiana kwa uvumilivu, wema, upendo na urafiki.

Pamoja na kuwa mwanaume ndiye mwenye haki na madaraka ya juu kwa mwanamke na kwamba mwanamke anapaswa awe mtiifu kwa mumewe katika mambo yasiyokuwa ya kumuasi Mwenyezi Mungu mtukufu, Mke pia ana haki zake chungu mzima, ambazo mume anatakiwa kuzitekeleza na kuzilinda, hivyo mwanaume anatakiwa asiwe mkorofi bali awe mpole, mwenye huruma kwa mkewe na amtimizie mahitaji yake yote. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

20.HAKI YA MTUMISHI:

Haki ya mtumishi ni kwamba: unatakiwa ufahamu umuhimu wake unatakiwa ufahami kwamba yeye ni mwanadamu kama wewe anaviungo, damu na hisia kama zako, na pia ufahamu kuwa wewe ni tajiri wake tu wala si muumba wake na wala wewe sio unayempa riziki, bali Mwenyezi Mungu mtukufu ndiye anayempa riziki wewe ni njia tu ya kupitia riziki hizo naye ni amana ambayo Mwenyezi Mungu mtukufu amekukabidhi, ili uilinde na kuihifadhi, hivyo muheshimu, mlinde na umtunze kama amana ya Mwenyezi Mungu kwako.

Mfanyie yale unayopenda kufanyiwa, mlishe unachokula, mvishe unachovaa, usimlazimishe wala kumkalifisha kufanya asiyoyaweza, kama humtaki basi usimuadhibu wala kumuudhi bali muache huru, na umuajili mwingine, Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

HAKI YA NDUGU NA JAMAA:

21.HAKI YA MAMA:

Haki ya mama ni kwamba: yakupasa ufahamu na kutambua umuhimu wake kwako, ufahamu na kukumbuka kwamba mama ndiye aliyekubeba tumboni muda mrefu kiasi ambacho, kinyume na mama hakuna atakaye kubali au kuwa radhi kukubeba kwa muda huo,na amekunywesha maziwa yake kwa furaha na ridhaa na kukulinda na kukutunza kwa kutumia nguvu na uwezo wake wote, kiasi ambacho hakuna mtu kinyume naye, mwenye kuweza kustahamili kukufanyia hivyo, hayo yote aliyafanya kwa ridhaa,furaha, uvumilivu na moyo mkunjufu na wala hakuwa na ajizi wala kuhisi uchovu wala kuchoshwa na malezi yako.

Mama ndiye mtu pekee aliyekuwa radhi kushinda njaa ili wewe ushibe, alikuwa tayari akose maji ili wewe unywe, mama ni mtu ambaye alikununulia wewe mavazi mapya naye akabaki na yazamani, mama ni mtu ambaye alikuwa tayari kuungua kwa jua, ili wewe upate kivuli, mama ni mtu ambaye alivumilia taabu na mashaka chungu mzima, ili wewe upate furaha na upate malezi bora, mama ni mtu pekee aliyekubembeleza ulale, na upate usingizi kwanza ndipo naye alale.

Tumbo lake lilikuwa nyumba yako, na alitumia maziwa yake kukulisha wewe, yeye ndiye alikuwa mlinzi na kimbilio lako, alivumilia taabu na mashaka, joto na baridi, ili wewe usipate taabu na uwe katika amani.

Hivyo mshukuru mama, fahamu na kutambua umuhimu wa mama, hakuna uwezo wala thamani ya kumlipa mama. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

22.HAKI YA BABA:

Haki ya baba ni kwamba: unatakiwa ufahamu kwamba baba ndiye asili na mizizi ya uwepo wako nawe ni kama matawi yake, bila baba wewe usingekuwepo, hivyo kila unapojitazama na kuona neema au kitu cha kukupendeza na kukufurahisha kumbuka kuwa, baba ni ndiye asasi na msingi ya neema na kitu hicho, mshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa neema zote alizokupatia, pia mshukuru baba yako kwa wema, neema na hisani zake kwako, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

23.HAKI YA MTOTO:

Haki ya mtoto ni kwamba: yakupasa ufahamu kwamba yeye ni mwanao na anatokana nawe na kwamba matendo yake mema au maovu yananasibishwa nawe katika ulimwengu huu, na kwamba ni jukumu lako kumfundisha maadili mema, na kumpa mafunzo ya dini na kumfahamu Mwenyezi Mungu mtukufu, unapaswa umuongoze, umsaidie na umuhimize mwanao kutekeleza na kufuata amri za Mwenyezi Mungu mtukufu, na ujue kuwa unapata thawabu kama utatekeleza wadhifa wako kwa mwanao na utapata dhambi na kuadhibiwa kama utazembea kutekeleza wadhifa wako kwake.

Hivyo fanya juhudi zako zote kumlea na kumpa malezi bora mwanao,kwani malezi bora na tabia njema za mwanao ndio pambo lako la hapa duniani na pia itakuwa ni sababu ya wewe kupata thawabu na malipo mema kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

24.HAKI YA NDUGU:

Haki ya ndugu yako ni kwamba: unatakiwa ufahamu kwamba ndugu yako ndiyo msaidizi wako, ndio nguvu yako, ndio kimbilio na tegemeo lako, na mtetezi wako dhidi ya maadui, hivyo jiupeshe usije tumia uwepo wake na uwezo wake katika maasi na mambo yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu mtukufu na wala usitumie msaada na utetezi wake katika kufanya dhulma na kupokonya haki za watu, una takiwa umsaidie na kumpa nasaha na umuepushe na maovu, na umsaidie kukabiliana dhidi ya mahasimu na maadui zake, inakupasa umsaidie kama atakuwa katika haki na njia ya Mwenyezi Mungu mtukufu na kama atakuwa kinyume na sheria na amri za Mwenyezi Mungu mtukufu, basi hutakiwi kumsaidia kufanya maovu na badala yake umnasihi na kumuongoza njia, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

25.HAKI YA ALIYEKUFANYIA HISANI:

Haki ya aliyekufanyia hisani ni kwamba: yakupasa ufahamu na kutambua kuwa ametumia mali zake katika kukufanyia hisani na kukuacha huru kutokana na kifungo na cha hali uliyokuwa nayo, na akuzawadia furaha ya uhuru na heshima, ametumia mali na ulimi wake kukufanyia hisani na kukutoa katika dhiki na matatizo ya utumwa uliokuwa nao, hivyo fahamu kuwa yeye ni mtu wa muhimu sana katika maisha yako baada ya ndugu zako na anahaki kubwa kwako mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu, basi jitahidi kuwa karibu naye na kumsaidia anapokuhitaji.

26.HAKI YA ALIYEFANYIWA HISANI:

Haki ya aliyefanyiwa hisani ni kwamba: unatiwa ufahamu kwamba ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyekupa uwezo wa kumfanyia hisani na

kumsaidia na wewe ulikuwa ni njia tu na sababu ya hisani hiyo kutimia, hivyo kutokana na kumfanyia hisani na kumuacha huru mtu mwenzako, Mwenyezi Mungu mtukufu, atakulipa mema duniani na anakuepusha na adhabu ya moto wa Jahannam siku ya Kiyama, pia Mwenyezi Mungu mtukufu amekupa haki ya kurithi mali zake, kama hata kuwa na ndugu wa kumrithi, hii inatokana na hisani ulomfanyia. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

27. HAKI YA MFADHILI:

Haki ya mfadhili ni kwamba: unatakiwa ufahamu umuhimu wake ukumbuke fadhila zake na kumshukuru na utaje na kumkumbuka kwa wema na ujitahidi kumfanyia wema kwa kadri ya uwezo wako na uwe karibu nawe na kumsaidia anapokuwa na shida au matatizo.

28. HAKI YA MUADHINI:

Haki ya muadhini ni kwamba: unatakiwa kukumbuka kuwa muadhini anakukumbusha Mola wako, na anakuita uelekee katika rehema za Mwenyezi Mungu mtukufu, na ufahamu kuwa yeye ni msaidizi wako mkuu anayekukumbusha utekeleze wajibu wako uliofaradhishiwa na Mwenyezi Mungu mtukufu, hivyo utakiwa ufahamu umuhimu wake na kumshukuru na umshukuru kwa wema aliyokufanyia, na wala usimtaje vibaya na ukumbuke kuwa uwepo wake ni rehema ya Mwenyezi Mungu kwako, hivyo shukuru na kuitukuza neema hii uliyopewa na Mwenyezi Mungu mtukufu. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

29.HAKI YA IMAMU:

Haki ya imamu ni kwamba: inatakiwa ufahamu na kutambua kuwa imamu wako wa sala, ni kiongozi na balozi baina yako na Mwenyezi Mungu mtukufu, na amesimama na kuwa katika nafasi hiyo kwa ajili ya kukuongoza na kukuwakilisha. Inabidi ufahamu uwepo na umuhimu wake kwamba yeye anakusalisha lakini wewe sio unayemsalisha, yeye anaomba dua kwa niaba yako, lakini wewe huombi kwa niaba yake na kwamba yeye ndiye msimamizi na kiongozi wa sala mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu, lakini wewe si kiongozi wa sala na ikiwa atakosea huesabika yeye ndiye sababu, na sio wewe na yeye ndiye atakayechukua jukumu la makosa hayo na sio wewe.

Hivyo unatakiwa ufahamu kuwa imamu wako wa sala amechukua jukumu zito sana, ameikoa sala yako kwa sala yake na kukulinda, basi yakupasa umshukuru kutokana na wadhifa wake kwako. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

30.HAKI YA MWENZI:

Haki ya mwenzi wako ni kwamba, uwe ni mwema kwa mwenzako, uwe mpole na mwenye huruma na kupatana nae, na umtendee haki na usawa katika mazungumzo usiwe mzunguzaji peke yako bali naye umsikilize na kumjali, unapokuwa naye usimuache peke yake bila ya ridhaa yake, na anapokuwa nawe pia asikuache peke yako ila baada ya ridhaa yako. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

31.HAKI YA JIRANI:

Haki ya jirani ni kwamba: unatakiwa umlindie mali na heshima yake kipindi hayupo na anapo kuwepo, na umsaidie panapohitajika sawa sawa awepo au asiwepo, na wala usimfuatilie na kutaka kuchunguza aibu na mambo yake, na ikiwa itatokea ukafahamu aibu au mambo yake ya siri kwa bahati mbaya na bila kukusudia kufanya ujasusi kwake, basi ni wadhifa wako kumtunzia siri na aibu zake kwa hali na mali, mpaka unahakikisha mtu mwingine hafahamu aibu na siri za jirani yako.

Pia unatakiwa umsaidie na wala usimuache peke yake akiwa kwenye matatizo, usimfanyie uhasidi, uadui, wala kumuonea wivu anapopewa neema na Mwenyezi Mungu mtukufu, msamehe makosa yake na yafasiri vizuri maneno yake, na ikitokea akakufanyia khiyana basi kuwa mvumilivu na zungumza naye kwa amani, usimlipe ubaya na jitahidi uishi na majirani zako kwa amani daima dawamu, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

32.HAKI YA SWAHIBA:

Haki ya swahiba wako ni kwamba: unatakiwa uishi naye vizuri na ushirikiane naye katika mema, na uongee naye mambo muhimu yenye faida, hivyo unatakiwa ufaidike na mema yake, naye afaidike na mema yako na umjali na kumtunzia heshima kama vile unavyopenda kujaliwa na kutunziwa heshima yako.

Jitahidi uwe mbele yake katika kufanya mema na ikitokea yeye akakuzidi katika kufanya mema, basi jitahidi nawe umzidi na muwe na ada na tabia yakushindana kufanya na kufanyiana mema, unatakiwa umpe nasaha swahiba wako na umlinde na uwe karibu nae na kumsaidia kwa hali na mali,

ila ukumbuke kuwa hutakiwi kumsaidia katika maasi na madhambi, bali watakiwa umzuie na kumkataza kufanya maasi, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

33.HAKI YA MSHIRIKA:

Haki ya mshirika wako ni kwamba: anapokuwa hayupo, ushike nafasi zake na kumsaidia na anapokuwepo mshirikiane kwa wema, asilani usifanye jambo bila ya kushauriana naye, nawala usitosheke na mtazamo wako pekee, mlindie mali zake, na usimfanyie khiyana katika mambo makubwa wala madogo, kwani wahenga wetu wametufunza kwamba:"Baraka za Mwenyezi Mungu ziko pamoja na wenye kushiriana vyema", Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

34.HAKI YA UTAJIRI:

Haki ya utajiri na mali ulizo nazo ni kwamba: usitafute utajiri wala mali kwa njia za utapeli na udanganyifu na wala usiutafute kwa njia zote zisizo halali na wala usiutumie utajiri na mali zako katika njia zisizo halali, bali uutumie utajiri na mali zako katika njia zenye manufaa ya dunia na akhera.

Usiwe bahili wa mali zako wala usijinyime na kuacha kuzitumia kwa matumizi muhimu yenyefaida kwa dunia na akhera yako, na kuhifadhi utajiri wako kwa ajili ya mrithi wako, ambaye yamkini akautumia vibaya utajiri huo, katika hali hii utahesabika kuwa umeshirikiana naye katika dhambi na maasi hayo, na ikiwa mrithi wako atautumia vyema utajiri wako basi nawe utapata thawabu na malipo toka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, Katika

kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

35.HAKI YA MWENYE KUDAI:

Haki ya mtu anayekudai ni kwamba: muda wa ahadi ya kulipa deni lako ufikapo basi umlipe bila kuchelewa wala kumsumbua kwani ni makosa kucheleweshа na kukaa na mali za watu. Mtume Muhammad s.a.w anasema: “Kwa mwenye uwezo, kuchelewa kulipa deni lake ni dhulma”. Na kama hauna uwezo wa kulipa kwa muda mliyo kuwa mmekubaliana usimkimbie, usimsumbue wala kumpa ahadi za uongo kwani utakuwa unamtaabisha na kumpotezea muda wake, bali ongea naye kwa upole na umuombe akupe muda wa kulipa deni hilo. Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

36.HAKI YA UNAEISHI NAYE:

Haki ya unaoishi naye pamoja ni kwamba: unatakiwa usimdhuru, usimdanganye, usimlaghai wala kumfanyia hiana , pia epukana na kila aina ya maudhi na madhila kwake na muishi kwa wema na amani, usimfanyie miamala ya kiadui, jitahidi umlinde na uwe mwaminifu kwake. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

37.HAKI YA MSHTAKI:

Haki ya mshtaki ni kwamba: ikiwa anaye kushtaki, madai yake dhidi yako ni sahihi na yakweli, na kwamba yeye ndiye mwenye haki, basi hautakiwi kutumia udanganyifu kwa kutaka kuthibisha kwamba madai na mashtaka

yake ni batili na hayana hoja wala dalili,kwani kufanya hivyo kuna hesabika ni kupingana na yaliyomo ndani ya nafsi yako, kwani wewe unajuafika kabisa kwamba wewe haupo katika haki na kwamba wewe unahatia, hivyo shauri jema ni kukiri na kukubaliana na madai ya mshtaki, kwani kukubali ukweli ni moja kati ya wadhifa wa waja wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

Na ikiwa madai na mashtaka yake si yakweli, hapo watakiwa kutetea haki yako, watakiwa ukumbushe amuogope Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kukusingizia na kukuweka hatiani, mkumbushe ajue kuwa kitendo cha kumsingizia mtu makosa ambayo hakuyafanya ni dhambi kubwa na atapata adhabu kali, katika kuthibitisha ukweli na kutetea haki yako, jiepushe na matumizi ya lugha chafu na kauli zisizo na maadili, kwani lugha chafu na kauli mbaya, huwa haziondoi bali huzidisha uadui na kuamsha hasira, za adui na hasimu wako, lakini maneno mazuri, maneno ya busara huondoa uadui na shari. Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

38.HAKI YA MSHITAKIWA:

Haki ya mshitakiwa ni kwamba: ikiwa wewe mwenye kushitaki upo katika haki, na kwamba madai na mastaka yako ni sahihi na yakweli, basi unatakiwa uzungumze na mstakiwa kwa adabu na upole, kwani kwa kufanya hivyo utatuzi wa tatizo utakuwa rahisi, kwa kutumia lugha mbaya mashtaka hayafutiki, bali humzidishia hasimu wako hasira, hivyo shauri jema ni kwamba; unatakiwa kutumia hoja madhubuti na lugha nzuri katika kuthibitisha na kutetea haki yako, na kama mshitakiwa atahitaji muhula na muda wa kutafakari basi mpe fursa hiyo.Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

39.HAKI YA MWENYE KUOMBA USHAURI:

Haki ya mwenye kukuomba ushauri ni kwamba: kama utakuwa na ushauri mzuri wa kumfaa basi usisite kumpatia ushauri huo, na umuonyeshe njia nzuri ambayo kama wewe ungekuwa nafasi yake basi ungeifuata njia hiyo, unatakiwa umshauri kwa kutumia lugha nzuri ya upole, kwani lugha nzuri na maneno ya upole, huondoa hofu katika moyo wake na kuweka matumaini, na kinyume chake ni kwamba maneno na lugha ya ukali humuondolea matumaini na kumpa hofu.

Na kama hautakuwa na ushauri wa kumpa, na unamfahamu mtu mwaminifu ambaye unaamini naweza kumsaidia, basi mpeleke kwa mtu huyo ili aweze kumshauri, kwa kufanya hivi utakuwa hujazembea na umetekeleza wadhifa wako. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

40.HAKI YA MSHAURI:

Haki ya mwenye kukushauri ni kwamba: kama itatokea ushauri alikupa hauafikiani na maoni yako, na wala haujaridhika na ushauri wake, basi usimtuhumu na kumuona kuwa ni mtu asiyefaa, kwani mitazamo na fikra za wanadamu zinatofautiana, na kutofautiana kimitazamo kwa wanadamu ni jambo la kawaida.

Lakini pia usisahau kwamba wewe ni mtu huru katika kuchagua, hivyo unaweza kubali ushauri au kuukataa, hivyo unapoona ushauri waendana na manufaa na maslahi yako, unahaki ya kuukubali, na unapoona haufai unahaki ya kuupinga, lakini si sahihi kumtuhumu aliyekushauri na kumuona kuwa ni mtu asiyefaa kwa kuwa amekupa ushauri unaopingana na rai yako.

Na ikitokea ushauri wake ukawa ni bora kwako na unaendana na kile ulichokuwa unakihitaji, basi Mshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu na

umshukuru mshauri wako, na ikitokea siku naye akaja kwako kuomba ushauri basi nawe mshauri kwa wema. Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

41. HAKI YA MWENYE KUOMBA NASAHA:

Haki ya mwenye kukuomba nasaha ni kwamba: unatakiwa umpe nasaha sahihi na zenye muongozo na umpe nasaha ambazo ataweza kuzifanyia kazi, usimpe nasaha ambazo ziko juu ya uwezo wake, na umpe nasaha zinazoendana na upeo wa akili yake ambazo itakuwa ni vyepesi kwake kuzifahamu, kwani wanadamu wote hawana uwezo mmoja katika kufikiri na kuelewa, bali kila mwanadamu ana uwezo wake wa kuelewa na kufikiri na umnasihi na kumpa nasaha kwa maneno laini na lugha nzuri ya upole. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

42. HAKI YA MWENYE KUTOA NASAHA:

Haki ya mwenye kutoa nasaha ni kwamba: uwapo mbele ya mwenye kukupa nasaha,uwe mwenye adabu na unyenyekevu,moyo wako uwe tayari kusikiliza nasaha zake, na umsikilize kwa makini ili upate kumuelewa, na baada ya kupokea nasaha, tumia muda kutafakari kunako nasaha hizo na ukiona zinamanufaa kwako basi usisite kuzifuata, na umshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa neema aliyokupatia.

Na ikitokea baada ya kutafakari ukaona kuwa nasaha zake si sahihi, basi usimuwekee kinyongo na wala usimtuhumu kwani alikuwa na lengo la kukunasihi na si vinginevyo, nakama ulikuwa naelimu tangu mwanzo kuwa anayekupa ushauri si mtu mzuri mwenye maadili, hivyo hutakiwi kuzitilia maanani nasaha zake, Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

43.HAKI YA WAKUBWA ZAKO:

Haki ya wakubwa zako na watu waliyo kuzidi cheo au umri ni kwamba: unatakiwa umuheshimu na uheshimu ukubwa wake kwako napia mheshimu na kutukuza kwa cheo chake au kukutangulia kwake katika uislamu na mambo mengine yanye fadhila kwa ubinadamu, mtangulize mbele kila mara na usibishane naye, usimtangulie katika kutembea, na ikitokea jambo halijui nawe walijua basi usimfedheheshe, na ikitokea akajifanya anajua basi zingatia mafunzo ya kiislamu yanayokutaka uwe mvumilivu kwake kwani amekuzidi umri. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

44.HAKI YA WADOGO ZAKO:

Haki ya wadogo zako na watu uliowazidi cheo na umri ni kwamba: unatakiwa uwe mpole kwao na ujitahidi kuwafundisha na kuwaelekeza yenye wema, manufaa na maadili, unatakiwa kufumbia macho makosa yako na kusitiri aibu zao, unatakiwa uishi na kufanya nao muamala mwema na uwasaidie katika matatizo na shida zao, pia vumilia makosa yao kwani ni wadogo zako na wanahitaji huruma yako, jiupueshe na mizaha, malumbano na ugomvi kwani husababisha athari mbaya kwa wadogo zako. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

45.HAKI YA MWENYE KUOMBA MSAADA:

Haki ya mwenye kukuomba msaada ni kwamba: kama unawezo wa kumsaidia basi msaidie kiasi cha kuondoa kabisa matatizo yake na kama hauna basi kwa kadri ya uwezo wako na umuombee dua, Mwenyezi Mungu mtukufu amuondolee matatizo yake.

Na kama utakuwa na mashaka na anayekuomba kwamba yamkini akawa ni tapeli au hana shida kama anavyodai, kama hautakuwa na uhakika kuwa ni tapeli au ni muongo, basi usiitilie maanani shaka yako, kwani huenda ikawa ni mbinu za shetani anakushawishi ili usisaidie wanaohitaji, ili ukose thawabu na ukose kuwa karibu na Mola wako.

Nakama shaka yako itaondoka na ukawa umemsaidia basi fahamu kuwa umetenda amali njema.

Na ikitokea hauna cha kumpa aliyekuomba, basi mpoze kwa maneno mazuri yenye upole, Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

46.HAKI YA UNAYE MUOMBA MSAADA:

Haki ya unayemuomba msaada ni kwamba: kama atakupa msaada basi mshukuru na kumuombea dua, na kama ikitokea bahati mbaya hajakupa msaada, basi kubali udhuru wake, usimuwekee kinyongo wala kumdhania vibaya. Na unatakiwa utafahamu kwamba alikuwa na uwezo wa kukusaidia, na hajakusaidia makusudi, basi hatakiwi kulaumiwa kwani ni mali yake na kwa kawaida mtu huwa halaumiwi kwa kutogawa mali yake kwa wengine. Na ikiwa atakunyima kwa ukaidi na udhalimu basi inakupasa kufahamu kwamba; si wanadamu wote wanaokumbuka kutoa na kushukuru kwa neema wakizopewa na Mwenyezi Mungu mtukufu. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

47.HAKI YA MWENYE KUKUFURAHISHA:

Haki ya mtu ambaye Mwenyezi Mungu mtukufu amemfanya kuwa ni sababu ya wewe kufurahi ni kwamba: ikiwa alikuwa na lengo la kukufurahisha na akakufurahisha, basi Mshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa neema hiyo, na umshukuru aliyekufurahisha kwa kukufurahisha, na unatakiwa nawe ujitahidi uwesababu ya yeye kufurahi na umfurahishe.

Na ikiwa amekufurahisha kwa sadfa bila kukusudia, basi mshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu na ufahamu kuwa hii ni neema kutoka kwake, aliyokupatia, na unatakiwa umpende na kumshukuru aliyekufurahisha, kwani amekuwa ni njia ya neema za Mwenyezi Mungu mtukufu kukufikia wewe, hata kama halikuwa kusudio lake, Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

48.HAKI YA ALIYEKUTENDEA UBAYA:

Haki ya aliyekuyekutendea ubaya ima kwa vitendo yake au kwa kauli yake, ni kwamba: ikiwa amekutendea ubaya kwa nia mbaya na kukusudia basi shauri jema ni kwamba; unatakiwa umsamehe, kwani msamaha wako utamfanya ajihisi aibu na itakuwa ni sababu ya yeye kutorudia tena kosa lake na kubadilika, na jitahidi uishi nae bila kinyongo.

Kwani Mwenyezi Mungu mtukufu katika Qur an tukufu surat Shuraa:41-43 anasema kwamba:

وَلَمَنِ انتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَٰئِكَ مَا عَلَيْهِم مِّن سَبِيلٍ

Na wanao jitetea baada ya kudhulumiwa, hao hawana lawama.

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۚ أُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

Bali lawama ipo kwa wale wanao wadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Watu hawa watapata adhabu kali.

وَلَمَن صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ

Na anaye subiri, na akasamehe, hakika hayo(kusubiri na kusamehe) ni katika mambo ya mema.

Pia Mwenyezi Mungu mtukufu katika suratu Nahl: 126 anasema kwamba:

وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُم بِهِ ۖ وَلَئِن صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ لِّلصَّابِرِينَ

"Na kama mkiadhibu, basi adhibuni sawa na vile mlivyoteswa; lakini kama mkisubiri, hakika hiyo ni bora zaidi kwa wanaosubiri"

Hii yote kama mtu atakufanyia ubaya kwa makusudi lakini kama atakufanyia ubaya bila kukusudia, unatakiwa umsamehe na hautakiwi kuadhibu au kulipa kisasi cha makudi kwa kosa lisilokusudiwa. Katika kutekeleza jukumu hili, tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

49. HAKI ZA WAISLAMU:

Haki ya waislamu wenzako ni kwamba: unatakiwa ufahamu kuwa waislamu wote ni ndugu, hivyo unapaswa kuishi nao kwa amani na huruma, uwe mpole kwa wanaokukosea, na uwakosoe kwa upole na huruma na mpendane nao, na washurukuru wenye kukufanyia wema, wafanyie hisani kwani kuwafanyia hisani wao ni sawa na kujifanyia hisani wewe mwenyewe, na usiwaudhi wala kuwa karahisha.

Hivyo unapaswa uwaombee dua waislamu wenzako wote, na uwasaidie na kuwa kirimu panapohitajika na kwa kadri ya uwezo wako. Katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

50.HAKI YA WASIO KUWA WAISLAMU:

Haki ya wasio kuwa waislamu ambao hawafanyi njama na wala hawafanyi uadui dhidi ya waislamu, nikwamba unatakiwa kuishi nao kwa amani na kuwatekelezea haki zao, ambazo Mwenyezi Mungu mtukufu amewawekea, na kufanya miamala nao kwa mujibu wa sheria ya Mwenyezi Mungu mtukufu. Msiwadhulumu wala kuwafanyia uadui.

Mtume Muhammad s.a.w anasema kwamba:

“yeyote atakayemdhulumu asiyekuwa muislamu, atakuwa kuwa amefanya uadui nami.”

Hivyo mwogopeni Mwenyezi Mungu mtukufu na muwe waadilifu katika mambo yenu,na katika kutekeleza jukumu hili tunategemea nguvu na uwezo wa Mwenyezi Mungu mtukufu.

Hizi ni haki za binadamu hamsini kutoka kwa imamu Zainul Abidin ambaye ni imamu wa nne wa madhehebu ya Shia ithna asharia. Unatakia kuzilinda na kuzifanyia kazi haki hizi, kwani haki hizi zimekusanya haki zote za binadamu na hauwezi kuepukana na haki hizi katika maisha yako ya kila siku. Tuna hitaji msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu kwani hakuna tegemeo wala kimbilio kwetu ila kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.